05

OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI
Sanduku la Barua, 2321, MMP, Zanzibar
Simu: +255242231869
Barua pepe: zanstat@ocgs.go.tz
Website: http://www.ocgs.go.tz

MAKAO MAKUU YA POLISI ZANZIBAR
Sanduku la Barua, 237
Baruapepe:cidphqznz@gmail.com
Nukushi: 024223136

# OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI ZANZIBAR

## TAKWIMU ZA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA ZANZIBAR KWA MWEZI WA MEI, 2023

# TOLEO LA TAKWIMU ZA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA - ZANZIBAR KWA MWEZI WA MEI, 2023

## UTANGULIZI

Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali imeandaa utaratibu ambao utawezesha ofisi kutekeleza majukumu yake iliyojipangia kuimarisha takwimu za jinsia. Miongoni mwa takwimu hizo ni kukusanya takwimu za matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia.

Toleo hili hutolewa kila mwezi ambalo hutoa muhtasari wa takwimu za maeneo mawili ya uhalifu ambazo ni ukatili na udhalilishaji wa kijinsia. Takwimu hizi zinatolewa kwa kutofautiana kwa kijiografia, kimakundi na kijinsia.

Takwimu za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia hutoa taarifa za idadi ya matukio yaliyotokea, aina ya waathirika na hali ya waathirika baada ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia. Takwimu hizo hutoa taarifa kuhusu matukio ambayo yameainishwa katika makundi makuu sita (6).


## LENGO

Lengo kuu la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia za ndani ya Zanzibar. Taarifa hizi ni muhimu na hutumiwa na wapangaji, watunga sera na watoa maamuzi.

## MATUKIO YA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA


Jumla ya matukio 154 ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia yameripotiwa mwezi wa Mei, 2023 ambapo waathirika walikuwa 154. Wengi wao walikuwa watoto sawa na asilimia 84.4,wanawake asilimia 10.4 na wanaume asilimia 5.2, miongoni mwa watoto wasichana walikuwa 108 (asilimia 83.1) nawavulana walikuwa 22 (asilimia 16.9).


Kielelezo 1.1 Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia Mei, 2023



Wilaya ya Magharibi "A imeripotiwa kuwa na matukio mengi ukilinganisha na wilaya nyengine (matukio 36) sawa na asilimia 23.4, ikifuatia wilaya ya Magharibi "B" ambapo yameripotiwa matukio 35 (asilimia 22.7).Wilaya ya Kusini imeripotiwa kuwa na idadi ndogo ya matukio kuliko wilaya zote ambapo tukio moja (1) sawa na asilimia 0.6.

**Kielelezo 1.2: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya Mei, 2023**




Idadi ya matukio kwa mwezi yameongezeka kwa asilimia 4.1 kutoka matukio 148 kwa mwezi wa Aprili, 2023 hadi 154 mwezi wa Mei, 2023. Wilaya ya Mjini iliripotiwa kuwa na matukio mengi ukilinganisha na wilaya nyengine (matukio 37) kwa mwezi wa Aprili, 2023 ambapo wilaya ya Magharibi "A" imeripotiwa kuongoza zaidi kwa mwezi wa Mei, 2023 (matukio 36).

**Jadweli 1.1: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya Mwezi Aprili, 2023 na Mwezi wa Mei, 2023**

| Wilaya | Idadi ya Matukio | | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia kinyume na maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | |
| | Aprili 2023 | Mei 2023 | Aprili 2023 | Mei 2023 | Aprili 2023 | Mei 2023 | Aprili 2023 | Mei 2023 | Aprili 2023 | Mei 2023 | Aprili 2023 | Mei 2023 | Aprili 2023 | Mei 2023 |
| Kaskazini 'A' | 4 | 8 | 1 | 3 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 3 | 2 | 1 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 10 | 4 | 6 | 2 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 3 | 0 |
| Kati | 9 | 14 | 4 | 7 | 0 | 1 | 3 | 5 | 1 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 |
| Kusini | 3 | 1 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Mjini | 37 | 31 | 14 | 12 | 7 | 2 | 0 | 0 | 1 | 1 | 3 | 2 | 12 | 14 |
| Magharibi 'A' | 35 | 36 | 19 | 18 | 2 | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 4 | 6 | 10 | 9 |
| Magharibi 'B' | 26 | 35 | 13 | 17 | 4 | 5 | 0 | 3 | 1 | 0 | 1 | 3 | 7 | 7 |
| Wete | 6 | 7 | 3 | 4 | 2 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 |
| Micheweni | 6 | 5 | 4 | 5 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 8 | 9 | 4 | 7 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 2 | 0 | 0 |
| Mkoani | 4 | 4 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 2 | 2 | 0 | 0 |
| **Zanzibar** | **148** | **154** | **72** | **76** | **20** | **13** | **4** | **9** | **4** | **5** | **16** | **21** | **32** | **30** |

Idadi ya matukio kwa mwaka yameongezeka kwa asilimia 108.1, ambapo jumla ya matukio yaloripotiwa kwa mwezi Mei, 2023 ni 154 wakati mwezi wa Mei, 2022 yaliripotiwa matukio 74. Wilaya ya Magharibi "A" iliripotiwa kuwa na idadi kubwa ya matukio kwa mwezi wa Mei, 2022 (matukio 16) ambapo pia Wilaya ya Magharibi "A" imeongoza kwa idadi kubwa ya matukio kwa Mei, 2023 (matukio 36).

Jadweli 1.2: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya, Mwezi Mei, 2022 na Mei ,2023

| Wilaya | Idadi ya Matukio | | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia kinyume na maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | |
| | Mei 2022 | Mei 2023 | Mei 2022 | Mei 2023 | Mei 2022 | Mei 2023 | Mei 2022 | Mei 2023 | Mei 2022 | Mei 2023 | Mei 2022 | Mei 2023 | Mei 2022 | Mei 2023 |
| Kaskazini 'A' | 2 | 8 | 1 | 3 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 5 | 4 | 4 | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 |
| Kati | 8 | 14 | 6 | 7 | 0 | 1 | 1 | 5 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 |
| Kusini | 1 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Mjini | 12 | 31 | 6 | 12 | 0 | 2 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 2 | 5 | 14 |
| Magharibi 'A' | 16 | 36 | 3 | 18 | 4 | 2 | 4 | 1 | 1 | 0 | 0 | 6 | 4 | 9 |
| Magharibi 'B' | 10 | 35 | 2 | 17 | 1 | 5 | 0 | 3 | 1 | 0 | 1 | 3 | 5 | 7 |
| Wete | 10 | 7 | 5 | 4 | 0 | 1 | 1 | 0 | 2 | 0 | 2 | 2 | 0 | 0 |
| Micheweni | 1 | 5 | 1 | 5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 5 | 9 | 3 | 7 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 |
| Mkoani | 4 | 4 | 2 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 2 | 0 | 0 |
| **Zanzibar** | **74** | **154** | **34** | **76** | **9** | **13** | **7** | **9** | **4** | **5** | **6** | **21** | **14** | **30** |

Miongoni mwa watoto 130 waathirika wa ukatili na udhalilishaji wa kijinsia; Wasichana waliobakwa walikuwa 69, Wavulana waliolawitiwa walikuwa 11, wasichana walioingilia kinyume na maumbile ni 9, Kutorosha walikuwa wasichana 5 , shambulio la aibu walikuwa 17 ambapo wasichana walikuwa 16 na mvulana mmoja (1) na shambulio walikuwa 19 ambapo wasichana walikuwa 9 na wavulana walikuwa 10.

Jadweli 1.3: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Wilaya Mei, 2023

| Wilaya | Idadi ya Matukio | Aina ya ukatili na udhalilishaji Zanzibar | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kulawiti | Kuingilia kinyume na maumbile | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | |
| | | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana |
| Kaskazini 'A' | 8 | 3 | 1 | 0 | 3 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 4 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 12 | 6 | 1 | 5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 23 | 11 | 2 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 4 | 4 |
| Magharibi 'A' | 28 | 15 | 1 | 1 | 0 | 0 | 5 | 0 | 3 | 3 |
| Magharibi 'B' | 29 | 15 | 4 | 3 | 0 | 0 | 2 | 0 | 2 | 3 |
| Wete | 7 | 4 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 |
| Micheweni | 5 | 5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 9 | 7 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 4 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 |
| **Zanzibar** | **130** | **69** | **11** | **9** | **5** | **0** | **16** | **1** | **9** | **10** |

Miongoni mwa wanawake 16 waathirika wa ukatili na udhalilishaji wa kijinsia; wanawake waliobakwa walikuwa ni saba (7), shambulio la aibu walikuwa wanawake watatu (3) na shambulio walikuwa wanawake sita (6).

Jadweli 1.4a: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake kwa Wilaya Mei, 2023

| Wilaya | Idadi ya Matukio | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kuingilia kinyume na maumbile | Kutorosha | Shambulio la Aibu/Kukashifu | Shambulio |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 2 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 5 | 1 | 0 | 0 | 1 | 3 |
| Magharibi 'A' | 5 | 3 | 0 | 0 | 0 | 2 |
| Magharibi 'B' | 4 | 2 | 0 | 0 | 1 | 1 |
| Wete | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chakechake | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Zanzibar** | **16** | **7** | **0** | **0** | **3** | **6** |

Jadweli 1.4b: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanaume kwa Wilaya Mei, 2023

| Wilaya | Idadi ya matukio | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Kulawiti | Kutorosha | Shambulio la Kukashifu | Shambulio |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 3 | 0 | 0 | 0 | 3 |
| Magharibi 'A' | 3 | 1 | 0 | 1 | 1 |
| Magharibi 'B' | 2 | 1 | 0 | 0 | 1 |
| Wete | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chakechake | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Zanzibar** | **8** | **2** | **0** | **1** | **5** |

Chanzo: Makao Makuu ya Polisi - Zanzibar

Watoto wenye umri wa miaka 15-17 imeripotiwa kuwa na idadi kubwa ya matukio (matukio 68) sawa na asilimia 52.3 ya matukio yote ya watoto yalioripotiwa ikifuatiwa na umri wa miaka 11-14 (matukio 33) sawa na asilimia 25.4. Aidha matukio ya kubaka yanaonesha kuwa mengi zaidi katika umri wa miaka 15-17(matukio 50) sawa na asilimia 72.5 ya matukio yote ya kubaka yalioripotiwa.

## Jadweli 1.5: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Wilaya Mei, 2023

| Miaka | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | | | | | | | | | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia kinyume namaumbile | | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | | |
| | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | |
| 0-5 | | 2 | 2 | | | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 0 | 0 | 8 |
| 6-10 | | 3 | 4 | | | 4 | 0 | 0 | 0 | 5 | 3 | 2 | 21 |
| 11-14 | | 14 | 4 | | | 2 | 0 | 1 | 0 | 6 | 3 | 3 | 33 |
| 15-17 | | 50 | 1 | | | 3 | 0 | 4 | 1 | 1 | 4 | 4 | 68 |
| **Jumla** | | **69** | **11** | | | **9** | **0** | **5** | **1** | **16** | **10** | **9** | **130** |

Chanzo: Makao Makuu ya Polisi - Zanzibar



Idadi ya watoto waathirika wa matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia kwa mwezi wa Mei, 2023 yameripotiwa kuwa na idadi sawa kwa mwezi wa Aprili na mwezi wa Mei, 2023. Mlinganisho wa idadi ya watoto waathirika wenye umri wamiaka 15- 17 kwa mwezi uliopita imeongezeka kwa asilimia 11.5 kutoka matukio 61 kwa mwezi Aprili, 2023 hadi matukio 68 kwa mwezi wa Mei, 2023.

**Jadweli 1.6: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Wilaya, Mwezi Aprili 2023 na Mei 2023**

| Miaka | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia kinyume na maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Shambulio | | Jumla Aprili 2023 | Jumla Mei 2023 |
| | Aprili 2023 | Mei 2023 | Aprili 2023 | Mei 2023 | Aprili 2023 | Mei 2023 | Aprili 2023 | Mei 2023 | Aprili 2023 | Mei 2023 | Aprili 2023 | Mei 2023 | | |
| 0-5 | 7 | 2 | 4 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 3 | 4 | 0 | 0 | 15 | 8 |
| 6-10 | 2 | 3 | 8 | 4 | 0 | 4 | 1 | 0 | 6 | 5 | 4 | 5 | 21 | 21 |
| 11-14 | 20 | 14 | 4 | 4 | 0 | 2 | 0 | 1 | 1 | 6 | 8 | 6 | 33 | 33 |
| 15-17 | 40 | 50 | 3 | 1 | 2 | 3 | 3 | 4 | 5 | 2 | 8 | 8 | 61 | 68 |
| **Jumla** | **69** | **69** | **19** | **11** | **3** | **9** | **4** | **5** | **15** | **17** | **20** | **19** | **130** | **130** |

Idadi ya watoto waathirika kwa mwaka uliopita yameongezeka kutoka matukio 64 kwa mwezi wa Mei, 2022 hadi matukio 130 kwa mwezi wa Mei, 2023, ambapo idadi ya matukio katika umri wa miaka yote yameongezeka kwa mwezi wa Mei 2023.


Jadweli 1.7: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Wilaya Mwezi Mei ,2022 na Mei, 2023

| Miaka | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia kinyume na maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Shambulio | | Jumla Mei 2022 | Jumla Mei 2023 |
| | Mei 2022 | Mei 2023 | Mei 2022 | Mei 2023 | Mei 2022 | Mei 2023 | Mei 2022 | Mei 2023 | Mei 2022 | Mei 2023 | Mei 2022 | Mei 2023 | | |
| 0-5 | 0 | 2 | 0 | 2 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 0 | 0 | 4 | 8 |
| 6-10 | 2 | 3 | 6 | 4 | 1 | 4 | 0 | 0 | 5 | 5 | 0 | 5 | 14 | 21 |
| 11-14 | 8 | 14 | 1 | 4 | 2 | 2 | 2 | 1 | 0 | 6 | 4 | 6 | 17 | 33 |
| 15-17 | 21 | 50 | 0 | 1 | 0 | 3 | 1 | 4 | 0 | 2 | 7 | 8 | 29 | 68 |
| **Jumla** | **31** | **69** | **7** | **11** | **7** | **9** | **3** | **5** | **5** | **17** | **11** | **19** | **64** | **130** |

Chanzo: Makao Makuu ya Polisi - Zanzibar

Matukio mengi zaidi yanaonesha kutokea nyumbani kwa mtuhumiwa (matukio 51) sawa na asilimia 33.1 ukilinganisha na maeneo mengine yaliyotajwa.

Kielelezo 1.3: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Sehemu Yaliyotokea Mei, 2023



Matukio 113 kati ya matukio 154 yameripotiwa yapo chini ya upelelezi wa Jeshi la Polisi sawa na asilimia 73.4, matukio 33 yapo Ofisi ya Mkurugenzi Mashtaka sawa na asilimia 21.4, matukio saba (7) yapo Mahkamani sawa na asilimia 4.6 na tukio moja (1) limefungwa na polisi sawa na asilimia 0.6.


**Jadweli 1.10: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Hatua Zilizochukuliwa Mei, 2023**

| Aina ya matukio | Idadi ya matukio | Waathirika | | | | Hatua zilizochukuliwa | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Mwanamme | Wanawake | Watoto | | Zilizo Mahakamani | Zilizotiwa hatiani | Ziliachiwahuru | Zilizofungwa Polisi | Zilizopelekwa kwa Ofisi ya M' mashtaka | Zilizo chini ya Upelelezi wa Polisi |
| | | | | Wasichana | Wavulana | | | | | | |
| Kubaka | 76 | | 7 | 69 | | 2 | 0 | 0 | 0 | 19 | 55 |
| Kulawiti | 13 | 2 | | | 11 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 9 |
| Kuingiliwa kinyume na maumbile | 9 | | 0 | 0 | | 3 | 0 | 0 | 0 | 2 | 4 |
| Kutorosha | 5 | 0 | 0 | 5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 5 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 21 | 1 | 3 | 16 | 1 | 2 | 0 | 0 | 1 | 3 | 15 |
| Shambulio | 30 | 5 | 6 | 9 | 10 | 0 | 0 | 0 | 0 | 5 | 25 |
| **Jumla** | **148** | **8** | **16** | **108** | **22** | **7** | **0** | **0** | **1** | **33** | **113** |

Chanzo: Makao Makuu ya Polisi - Zanzibar

Wafanyaji wa matukio ya ukatili na udhalilishaji wa Kijinsia walioripotiwa kwa mwezi wa Mei 2023 ni 154 kati yao 100 walikuwa wapita njia sawa na asilimia 64.9 kati ya watuhumiwa wote walioripotiwa.

Kielelezo 1.4: Aina ya Watu Waliofanya Matukio ya Ukatiki na Udhalilishaji wa Kijinsia Mei, 2023



## HITIMISHO

Takwimu za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia hutoa taarifa za idadi ya matukio yaliyotokea, aina ya waathirika na hali ya waathirika baada ya ukatili na udhalilishaji wa Kijinsia, muda wa matukio yalipotokea na wafanyaji wa matukio. Takwimu hizo hutoa taarifa kuhusu matukio ambayo yameainishwa katika makundi makuu sita (6). Lengo kuu la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia za ndani ya Zanzibar. Taarifa hizi ni muhimu na hutumiwa na wapangaji, watunga sera na watoa maamuzi.

Jumla ya matukio 154 ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia yameripotiwa mwezi wa Mei, 2023 ambapo Magharibi "A" imeripotiwa kuwa na idadi kubwa ya matukio ya kubaka ikilinganishwa na wilaya nyengine. Idadi ya matukio kwa mwezi yameongezeka kwa asilimia 4.1 kutoka matukio 148 kwa mwezi wa Aprili, 2023 hadi 154 mwezi wa Mei, 2023.

Matukio 113 kati ya matukio 154 yameripotiwa yapo chini ya upelelezi wa Jeshi la Polisi sawa na asilimia 73.4, matukio 33 yapo Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka sawa na asilimia 21.4, matukio saba (7) yapo Mahkamani sawa na asilimia 4.6 na tukio moja (1) limefungwa na polisi sawa na asilimia 0.6.

## Kiambatanisho

### Jadweli 1.0: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Maeneo yaliyofanyika Matukio Mei, 2023

| Eneo la matukio | Kubaka | | | Kulawiti | | | Kuingilia kinyume na maumbile | | | Kutorosha | | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | | Shambulio | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla |
| Nyumbani kwa Muathirika | 1 | | 1 | | 0 | 0 | 1 | | 1 | 3 | 0 | 3 | 2 | 0 | 2 | 7 | 8 | 15 |
| Nyumbani kwa Mtuhumiwa | 24 | | 24 | | 5 | 5 | 5 | | 5 | 0 | 0 | 0 | 8 | 0 | 8 | 5 | 4 | 9 |
| Nyumba za wageni/kwarafiki | 11 | | 11 | | 1 | 1 | 0 | | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Sehemu za kazi | 0 | | 0 | | 0 | 0 | 0 | | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 2 | 4 |
| Skuli/ Madrasa | 0 | | 0 | | 0 | 0 | 0 | | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Majumba mabovu | 15 | | 15 | | 2 | 2 | 2 | | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Sehemu nyengine(Vichakani na kwengine) | 25 | | 25 | | 5 | 5 | 1 | | 1 | 2 | 0 | 2 | 9 | 2 | 11 | 1 | 1 | 2 |
| **Jumla** | **76** | | **76** | | **13** | **13** | **9** | | **9** | **5** | **0** | **5** | **19** | **2** | **21** | **15** | **15** | **30** |

Chanzo: Makao Makuu ya Polisi - Zanzibar

Jadweli 1.12: Mlinganisho wa Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Maeneo yaliyofanyika Matukio kwa mwezi Aprili, 2023 na Mei, 2023

| Eneo la matukio | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia kinyumena maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Shambulio | | Jumla Aprili 2023 | Jumla Mei 2023 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Aprili | Mei | Aprili | Mei | Aprili | Mei | Aprili | Mei | Aprili | Mei | Aprili | Mei | | |
| Nyumbani kwa Muathirika | 3 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 3 | 2 | 2 | 10 | 15 | 16 | 22 |
| Nyumbani kwa Mtuhumiwa | 27 | 24 | 7 | 5 | 4 | 5 | 2 | 0 | 7 | 8 | 15 | 9 | 62 | 51 |
| Nyumba za wageni/kwa rafiki | 5 | 11 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 5 | 12 |
| Sehemu za kazi | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 1 | 4 |
| Skuli/ Madrasa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Majumba mabovu | 11 | 15 | 4 | 2 | 0 | 2 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 17 | 19 |
| Sehemu nyengine(Vichakani na kwengine) | 27 | 25 | 10 | 5 | 0 | 1 | 1 | 2 | 6 | 11 | 7 | 2 | 51 | 46 |
| **Jumla** | **74** | **76** | **21** | **13** | **4** | **9** | **4** | **5** | **17** | **21** | **32** | **30** | **152** | **154** |

Jadweli 2.0: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya Mei, 2023

| Wilaya | Idadi ya Matukio | Aina ya ukatili na udhalilishaji Zanzibar | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kulawiti | Kuingilia kinyume na maumbile | Kutorosha | Shambulio la Aibu/Kukashifu | Shambulio |
| Kaskazini 'A' | 8 | 3 | 1 | 0 | 3 | 1 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 4 | 2 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Kati | 14 | 7 | 1 | 5 | 0 | 1 | 0 |
| Kusini | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Mjini | 31 | 12 | 2 | 0 | 1 | 2 | 14 |
| Magharibi 'A' | 36 | 18 | 2 | 1 | 0 | 6 | 9 |
| Magharibi 'B' | 35 | 17 | 5 | 3 | 0 | 3 | 7 |
| Wete | 7 | 4 | 1 | 0 | 0 | 2 | 0 |
| Micheweni | 5 | 5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 9 | 7 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 |
| Mkoani | 4 | 1 | 0 | 0 | 1 | 2 | 0 |
| **Zanzibar** | **154** | **76** | **13** | **9** | **5** | **21** | **30** |

**Jadweli 3.0: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia, Mwezi Aprili, 2023 na Mei, 2023**

| Aina ya matukio | Idadi ya matukio | | Waathirika | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Wanawake | | Watoto | | | | Wanaume | |
| | | | | | Wasichana | | Wavulana | | | |
| | Aprili 2023 | Mei 2023 | Aprili 2023 | Mei 2023 | Aprili 2023 | Mei 2023 | Aprili 2023 | Mei 2023 | Aprili 2023 | Mei 2023 |
| Kubaka | 72 | 76 | 5 | 7 | 69 | 69 | | | | |
| Kulawiti | 20 | 13 | | | | | 19 | 11 | 2 | 2 |
| Kuingiliwa kinyume na maumbile | 4 | 9 | 1 | 0 | 3 | 9 | | | | |
| Kutorosha | 4 | 5 | 0 | 0 | 4 | 5 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 16 | 21 | 2 | 3 | 14 | 16 | 1 | 1 | 0 | 1 |
| Shambulio | 32 | 30 | 8 | 6 | 9 | 9 | 11 | 10 | 4 | 5 |
| **Jumla** | **148** | **154** | **16** | **16** | **99** | **108** | **31** | **22** | **6** | **8** |

**Jadweli 4.0: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia Mwezi Mei, 2022 na Mei ,2023**

| Aina ya matukio | Idadi ya matukio | | Waathirika | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Wanawake | | Watoto | | | | Wanaume | |
| | | | | | Wasichana | | Wavulana | | | |
| | Mei 2022 | Mei 2023 | Mei 2022 | Mei 2023 | Mei 2022 | Mei 2023 | Mei 2022 | Mei 2023 | Mei 2022 | Mei 2023 |
| Kubaka | 34 | 76 | 3 | 7 | 31 | 69 | | | | |
| Kulawiti | 9 | 13 | | | | | 7 | 11 | 2 | 2 |
| Kuingiliwa kinyume na maumbile | 7 | 9 | 0 | 0 | 7 | 9 | | | | |
| Kutorosha | 4 | 5 | 1 | 0 | 3 | 5 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 6 | 21 | 1 | 3 | 2 | 16 | 3 | 1 | 0 | 1 |
| Shambulio | 14 | 30 | 3 | 6 | 3 | 9 | 8 | 10 | 0 | 5 |
| **Jumla** | **74** | **154** | **8** | **16** | **46** | **108** | **18** | **22** | **2** | **8** |

Jadweli 5.0: Muda wa Matukio ya Udhalilishaji Yalipotokea Mei, 2023

| Muda | Kubaka | Kulawiti/Kunajis | Kuingilia Kinyume na Maumbile | Kutorosha | Shambulio la Aibu /Kukashifu | Shambulio | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 12:01 - 03:00 Asubuhi | 4 | 5 | 2 | 0 | 5 | 1 | 17 |
| 03:01 - 6:00 Mchana | 11 | 2 | 1 | 0 | 4 | 2 | 20 |
| 6:01 - 9:00 Jioni | 14 | 1 | 2 | 0 | 6 | 5 | 28 |
| 9:01 - 1200 Jioni | 8 | 3 | 1 | 2 | 3 | 8 | 25 |
| 12:01 - 3:00 usiku | 25 | 2 | 2 | 3 | 3 | 6 | 41 |
| 3:01 - 6:00 Usiku | 9 | 0 | 1 | 0 | 0 | 8 | 18 |
| 6:01 - 09:00 Usiku | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 |
| 09:01 - 12:00 Asubuhi | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 |
| **Jumla** | **76** | **13** | **9** | **5** | **21** | **30** | **154** |

## Zingatia Maelezo

Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia Kitendo chochote au mwenendo wowote, ambao husababisha moja kwa moja kwa mtu, kama mateso ya kimwili, ya kimapenzi au ya kiakili kupitia vitisho, kulazimisha au njia zingine; lengo la kutisha, kuadhibu, kuwadhalilisha, kudhoofisha usalama au kujiheshimu; kutosheleza hamu ya ngono; au kudhoofisha uwezo wa mwili au kiakili wa mtu kwa sababu ya jinsi yake. Kwa mfano, unyanyasaji wa kijinsia, kumpiga mke, unyanyasaji wa kijinsia wa wasichana na wavulana, ukeketaji wa kike, mwanamke kuua watoto wachanga, utoaji mimba, ukahaba wa kulazimishwa , Biashara haramu ya usafirishaji wa wanawake na watoto wa kike na ponografia (uenezaji wa ngono haramu).

Sheria ya Adhabu ya 6/2018 iliongeza adhabu kwa makosa yanayohusiana na maadili kama vile ubakaji, kulawiti, kuingilia kinyume na kimaumbile na shambulio la aibu;

Sheria hii imetungwa mwaka 2018 ambayo imekuja kufuta sheria kama hii ya mwaka 2004. Sheria hii imetungwa pamoja na mambo mengine kuyafanya baadhi ya matendo kuwa makosa ya jinai na kuyawekea adhabu zake endapo mtu yeyote atayatenda matendo hayo na mahkama itamuona ana hatia. Kwenye shehemu ya kumi na tatu (Section thirteen) ya sheria ya adhabu imejumuisha makosa mengi ambayo ni makosa dhidi ya vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto.

Sheria ya mwenendo wa Jinai 7/2018 kifungu cha 151 (1) kina vifungu ambavyo haviruhusu utoaji wa dhamana kwa mtu yeyote anayeshtakiwa kwa kesi zinazohusiana na ukatili na udhalilishaji wa kijinsia, pamoja na kuongezeka kwa hukumu ambazo Mahakama zinaweza kupitisha. Kwa mfano, katika Mahakama ya Mkoa kesi za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia kutoka miaka 7 hadi miaka 14 na kwa Mahakama Kuu kutoka miaka 30 hadi kifungo cha maisha.

**KWA UFAFANUZI ZAIDI TAFADHALI WASILIANA NA:**

OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI
Sanduku la Barua,2321, MMP, Zanzibar
Simu: +255242231869
Barua pepe: zanstat@ocgs.go.tz
Website: http://www.ocgs.go.tz

MAKAO MAKUU YA POLISI ZANZIBAR
Sanduku la Barua, 237, MMP,
Barua pepe:cidphqznz@gmail.com
Nukushi: 024223136